**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA (MB), WAZIRI WA MIUNDOMBINU KATIKA HAFLA YA UZINDUZI RASMI WA UJENZI WA BARABARA YA TANGA - HOROHORO TAREHE 28 MEI 2010**

Mheshimiwa, Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Waheshimiwa Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mheshimiwa, Meja Jen.Mst. Saidi Kalembo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga,
Mheshimiwa Alfonso E. Lenhardt, Balozi wa Marekani nchini Tanzania,
Mheshimiwa Daniel W. Yohannes, Rais wa Mfuko wa Changamoto za Millenia (MCC),
Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,
Waheshimiwa Wabunge,
Waheshimiwa Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa,
Wageni Waalikwa,
Ndugu Wananchi,
Mabibi na Mabwana.

**Mheshimiwa Rais,**

1. Awali ya yote ninaomba nikushukuru kwa kukubali mwaliko wetu wa kuja kuhudhuria na kuwa mgeni rasmi

katika sherehe hii ya uzinduzi rasmi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro. Ni dhahiri kuwa unayo majukumu mengi ya kitaifa na kimataifa, hata hivyo, umeridhia kutenga muda wako kuja kujumuika nasi katika sherehe hii muhimu kwa Wananchi wa mkoa wa Tanga na Taifa letu kwa ujumla. Tunakushukuru sana.

**Mheshimiwa Rais,**

2. Jukumu langu ni kukukaribisha ili uongee na Wananchi waliohudhuria katika sherehe hii, lakini kabla sijafanya hivyo, napenda kutumia nafasi hii kuelezea japo kwa kifupi umuhimu wa mradi huu:

   Barabara ya Tanga - Horohoro yenye urefu wa Kilometa 65 ambayo ujenzi wake utauzindua rasmi leo, ni sehemu ya barabara kuu ya Dar es Salaam – Tanga – Horohoro yenye urefu wa Kilometa 450. Barabara hii ni kiungo muhimu kwa mikoa ya ukanda wa pwani ya kaskazini mwa Dar es Salaam yaani Dar es Salaam, Pwani na Tanga.

   Aidha, barabara hii ni kiungo muhimu kati yetu na bandari ya Mombasa iliyopo kwenye mwambao wa pwani ya nchi jirani ya Kenya.

**Mheshimiwa Rais,**

3. Kama alivyotangulia kueleza Katibu Mkuu, ujenzi wa barabara hii unagharamiwa na Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCC). Kwa nchi za Afrika, Tanzania ndiyo nchi iliyotengewa kiasi kikubwa cha fedha ikilinganishwa na nchi nyingine katika bara hili. Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Serikali ya Marekani kupitia kwa Balozi wa Marekani nchini Mheshimiwa Alfonso Lenhardt na Rais wa *Millenium Challenge Corporation* Mheshimiwa Daniel Yohannes.

**Mheshimiwa Rais,**

4. Madhumuni ya ujenzi wa barabara hii ni kuimarisha mtandao wa barabara katika kuongeza uwezo na ufanisi na hivyo kuleta changamoto ya uchumi kwa kupunguza umasikini na gharama za usafirishaji katika maeneo yanayopitiwa na barabara. Aidha, mradi unatarajiwa kuboresha hali ya maisha kwa wananchi wanaoishi kando mwa barabara hii kwa kuondoa kero ya muda mrefu ya kutokuwa na miundombinu ya barabara ya uhakika na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii, usafirishaji wa pembejeo za kilimo na mazao ya wakulima kufika kwenye masoko kwa wakati.

**Mheshimiwa Rais,**

5. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCC) na usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Milenia Tanzania (MCA-T) ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya barabara za Songea hadi Namtumbo ambayo mkataba wake wa ujenzi umesainiwa tarehe 25 Mei, 2010 na Peramiho hadi Mbinga katika ukanda wa Mtwara (*Mtwara Corridor*) na barabara ya Tunduma hadi Sumbawanga katika Ukanda wa Magharibi (*Western Corridor*).

   Kwa upande wa barabara ya Tunduma - Sumbawanga ambayo ujenzi wake umegawanywa katika sehemu tatu, mkataba wa sehemu ya Laela - Sumbawanga ulisainiwa mwezi Machi, 2010 na tayari Mkandarasi ameanza kazi. Sehemu ya Tunduma - Ikana na Ikana - Laela mchakato wa kupata Makandarasi upo kwenye hatua za mwisho.

**Mheshimiwa Rais,**

6. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Ujenzi wa barabara ya Tanga - Horohoro unafanyika wakati tunaimarisha ushirikiano wa nchi za

Afrika Mashariki. Hivyo barabara hii itakapokamilika kujenga kwa kiwango cha lami, itasaidia kukuza biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani ya Kenya. Aidha, ujenzi wa barabara hii utamaliza kero ya wananchi wa mkoa wa Tanga ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakisubiri kwa hamu kubwa utekelezaji wa mradi huu. Baada ya fedha za ujenzi kupatikana na mkataba wa ujenzi kusainiwa, ni dhahiri kuwa sasa hakuna kitakachokwamisha utekelezaji wa mradi huu. Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara itasimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ili ukamilike kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa.

**Mheshimiwa Rais,**

7. Utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani chini ya Mfuko wa Changamoto ya Milenia ni matunda ya juhudi zako binafsi ambapo ulifanikiwa kuishawishi Serikali ya Marekani kutoa bilioni 700. Napenda pia kuwashukuru watendaji wote wa Mfuko wa changamoto ya Milenia walioshiriki katika maandalizi ya mradi huu hadi kufanikisha kupatikana kwa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri na leo hii tunashuhudia uzinduzi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Ni matarajio yetu kuwa Mkandarasi atatekeleza mradi kwa ubora na kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika mkataba.

**Mheshimiwa Rais,**

8. Nimalizie kwa kuwaomba Viongozi wenzangu wa Serikali katika Mkoa wa Tanga na Wananchi waishio kwenye maeneo yanayopitiwa na barabara hii, kutoa ushirikiano kwa Mkandarasi ili aweze kukamilisha ujenzi wa barabara hii muhimu kwa wakati uliopangwa.

   Uzoefu katika miradi mingine unaonyesha kuwa kumekuwa na wananchi wachache wenye tabia ya udokozi wa vifaa vya ujenzi na mali za Mkandarasi. Vitendo hivi vinachangia kuzorotesha ufanisi wa kazi na hivyo kuathiri kasi ya utekelezaji wa mradi. Kama na Tanga wapo, tunawaasa waache tabia hizo.

**Mheshimiwa Rais,**

9. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa nichukue nafasi hii kukukaribisha uzungumze na Wananchi na hatimaye uzindue rasmi ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro.

**MHESHIMIWA RAIS, KARIBU.**